26. Kutowajibishwa kwa utoaji wa taarifa.
27. Utoaji wa taarifa zisizo na utambulisho.
28. Usalama wa taarifa zilizorekodiwa.
29. Kuharibu fomu ya marejesho ya taarifa binafsi.
30. Mamlaka a kupata maelezo.
31. Upatikanaji wa kumbukumbu.

**SEHEMU YA NNE
MASUALA YA FEDHA**

32. Vyanzo vya mapato.
33. Makadirio.
34. Hesabu.
35. Ukaguzi.
36. Taarifa ya mwaka ya utekelezaji.

**SEHEMU YA TANO
MAKOSA NA ADHABU**

37. Makosa na adhabu.

**SEHEMU YA SITA
MASUALA YA JUMLA**

38. Kanuni.
39. Kufuta na kuhifadhi.
40. Kukinzana na Sheria nyingine.

MAJEDWALI

TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa kwa taarifa ya jumla kwa umma pamoja na madhumuni na sababu zake.

Dar es Salaam,
5 Juni, 2013

OMBENI Y. SEFUE
Katibu wa Baraza la Mawaziri

MUSWADA

Wa

Sheria ya kufuta Sheria ya Takwimu, kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu, na Bodi ya usimamizi wa takwimu, kuweka masharti yanayohusu uratibu wa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu, na kuweka masharti bora kuhusiana na majukumu ya Ofisi na Bodi, na masharti mengine yanayohusiana na hayo.

SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

Jina la Sheria
na tarehe ya
kuanza
kutumika

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Takwimu, 2013 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri anaweza, kwa taarifa itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kuiteua.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara katika masuala yote yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili na itatumika Tanzania Zanzibar kuhusiana na masuala ya Sensa ya Watu na Makazi.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

“wakala au mawakala” inajumuisha taasisi za utafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali, washirika wa maendeleo au watumiaji au wazalishaji wengine wowote wa takwimu;

“afisa aliyeidhinishwa” ina maana ya mtu aliyeteuliwa kwa maana hiyo chini ya kifungu cha 15;

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Taifa ya Takwimu iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7;

“ofisi” maana yake ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

- “Sensa” maana yake ni shughuli ya uchukuaji wa taarifa za watu au vitu vyote vinavyokusudiwa katika maeneo yote husika;
- “Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Takwimu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10;
- “taasisi za Serikali” inajumuisha Wizara, idara za Serikali na mamlaka za serikali za mitaa;
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya takwimu;
- “Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu” maana yake ni mfumo unaoratibiwa na Ofisi ambao unajumuisha watoa taarifa, wazalishaji au watumiaji wa takwimu, na taasisi za utafiti na mafunzo;
- “mtumishi” maana yake ni mtumishi yeyote aliyeajiriwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;
- “takwimu rasmi” maana yake ni takwimu zinazokubaliwa na kutambulika kuwa rasmi chini ya kifungu cha 20;
- “sensa ya watu na makazi” maana yake ni sensa inayoendeshwa na Ofisi ya Takwimu chini ya kifungu cha 21;
- “mlalamikiwa” maana yake ni mtu yeyote ambaye anatoa au anatakiwa kutoa taarifa za takwimu;
- “marejesho” maana yake ni kitabu chochote, nyaraka, fomu, kadi, kinasa sauti, santuri au kitu chochote ambacho kinahifadhi taarifa inayotakiwa kuingizwa au kurekodiwa au inahitajika kuingizwa au kurekodiwa kwa ajili ya shughuli za kitakwimu chini ya sheria hii;
- “sampuli” maana yake ni utaratibu wa kitakwimu ambapo taarifa zinazohusiana na eneo zima la utafiti zinapatikana kwa kutumia mbinu za kitakwimu zinazopatikana kuhusiana na uwiano wa idadi ya watu au vitu vilivyomo vinavyohusu eneo zima la utafiti;
- “takwimu” maana yake ni taarifa zinazohitajika kwa ajili ya kukusanya taarifa za kitakwimu, zinazopatikana kutokana na sensa na utafiti wa kitakwimu au kumbukumbu za kiutawala;
- “mtafiti” maana yake ni mtu anayefanya kazi ya kuhesabu takwimu;
- “kitengo cha utafiti” maana yake ni sehemu, kitengo au idara iliyoanzishwa chini ya wakala wowote anayehusika na utekelezaji wa kazi za kitakwimu;
- “utafiti” inajumuisha uchunguzi wa kitakwimu au watu ambao taarifa zinakusanywa kutoka watu wote katika utafiti unaofanywa au aina ya utafiti huo wote au

sehemu kwa madhumuni ya kitakwimu;
“kazi” ina maana ya shughuli yoyote ya kitakwimu kwa njia ya biashara iwapo au la biashara inaendeshwa kwa faida na inajumuisha Wizara au idara za Serikali, mamlaka za kisheria, serikali za mitaa, na aina nyingine yeyote ya taasisi au jumuiya ya watu au sehemu nyingine yeyote inayoendana nayo.

SEHEMU YA PILI
OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU NA BODI YA USIMAMIZI
(a) Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Muendelezo
wa Ofisi ya
Taifa ya
Takwimu

4.-(1) Itaendelea kuwepo Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambayo itajulikana kwa kifupi chake kama “NBS”.
(2) Ofisi itakuwa ni taasisi huru ya umma chini ya Wizara ya fedha.

Uadilifu wa
Ofisi

5. Kwa nia ya kulinda na kuendeleza uadilifu na uhakika wa takwimu, Ofisi ya Takwimu itafanya shughuli zake kwa uhuru na kitaaluma wakati wa kukusanya, kuchambua, kutathmini na kusambaza taarifa za kitakwimu.

Majukumu
ya Ofisi ya
Takwimu

6.-(1) Ofisi ya Takwimu itakuwa ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu inayowajibika na uzalishaji, uratibu, usimamizi na usambazaji, na utunzaji wa takwimu rasmi nchini.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), Ofisi -

- (a) itaendesha sensa ya watu na makazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
 - (b) itashauri serikali na umma kuhusu masuala yote yanayohusiana na takwimu na maendeleo ya kitakwimu;
 - (c) itatoa taarifa za kitakwimu kwa umma zenye ubora, uhakika na kwa wakati;
 - (d) itaandaa na kutunza katika sehemu moja taarifa za kitakwimu, machapisho, nyaraka na taarifa zote za ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano;
 - (e) itaandaa mbinu, viwango na tafsiri kwa ajili ya kutengeneza takwimu rasmi;
 - (f) itaratibu na kusimamia Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu nchini; na
 - (g) itatekeleza kazi zote muhimu au zinazoambatana kwa madhumuni ya Ofisi chini ya Sheria hii.
- (3) Ofisi, Katika kutekeleza majukumu yake, inaweza

kuingia mkataba na taasisi au mtu yeyote kwa kuzingatia vigezo na masharti kwa mujibu wa makubaliano ya wahusika.

(4) Ofisi kwa kazi zinazohusisha Tanzania Zanzibar, itafanya kazi hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(b) Bodi ya Usimamizi

Uanzishwaji
na Muundo wa
Bodi

7.-(1) Itaanzishwa Bodi ya Usimamizi ya Ofisi ya ofisi ya Takwimu itakayojulikana kama ya Bodi ya Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

(2) Bodi itakuwa na-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye taaluma na uzoefu wa masuala ya takwimu, hisabati, uchumi na uelewa katika masuala ya kibiashara na kiutawala; na

(b) wajumbe wengine sita, wenye vyeo vya Mwandamizi Mkuu au zaidi, watakaoteliwa na Waziri baada ya kuchaguliwa na asasi au taasisi husika kama ifuatavyo-

(i) mwakilishi wa Benki kuu;

(ii) mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya masuala ya takwimu;

(iii) mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iv) mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(v) mwakilishi kutoka Taasisi za Elimu ya Juu;

(vi) mjumbe mmoja atakayeteuliwa kutoka miongoni mwa watumiaji au wazalishaji wa takwimu kutoka sekta binafsi.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Bodi.

(4) Masharti ya Jedwali la kwanza yatumika kuhusiana na kipindi cha kuwepo kazini na kusitishwa kuwa mjumbe, shughuli za Bodi na mambo mengine yanayohusiana na Bodi.

Majukumu ya
bodi

8. Majukumu ya Bodi yatajumuisha-

(a) kuidhinisha na kufuatilia utekelezaji wa sera zinazoihusu Ofisi;

(b) kuamua mara kwa mara muundo, uendelezaji wa taaluma, kiwango cha watumishi na makubaliano na masharti kwa ajili ya watumishi wa Ofisi;

(c) kuhidhinisha uteuzi wa watumishi wa ngazi za

- utawala;
- (d) kuchukua hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi ya watumishi wa ngazi za utawala katika Ofisi;
 - (e) kuidhinisha mpango wa ofisi, mpango-kazi wa kila mwaka na bajeti ya mwaka;
 - (f) kumfahamisha Waziri maendeleo ya utendaji wa Ofisi kila baada robo ya mwaka; na
 - (g) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama yatakavyoelekezwa na Waziri kwa maandishi.

Uteuzi wa
Mkurugenzi
Mkuu

9.-(1) Rais atamteua Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu kufuatia mapendekezo ya Waziri.

(2) Mtu hatakuwa na sifa za kupendekezwa na kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu isipokuwa kama ana sifa za kuwa na shahada au taaluma nyingine zaidi ya shahada katika tasnia ya takwimu au Uchumi au Hisabati na awe angalau na uzoefu wa miaka kumi katika tasnia ya takwimu na pia awe amethibitika kuwa na uwezo wa kuongoza.

(3) Mkurugenzi Mkuu ataongoza ofisi kwa kipindi cha miaka mitano kwa kuzingatia utendaji wake wa kazi, na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Usitishwaji
wa uteuzi

10. Rais anaweza, baada ya mapendekezo ya Waziri, kusitisha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kutokana na-

- (a) utovu wa nidhamu;
- (b) kushindwa au kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya ofisi yake kutokana na udhaifu wa mwili au akili; au
- (c) kutokuwa na uwezo kiutendaji.

Kazi
Mkurugenzi
Mkuu

11. Mkurugenzi Mkuu atakuwa Mtendaji Mkuu wa Ofisi na atatakiwa kufanya kazi za Ofisi za kila siku ikiwa ni pamoja na kusimamia fedha, mali na shughuli za Ofisi na utawala, upangaji na udhibiti wa maofisa na watumishi wa Ofisi.

Kaimu
Mkurugenzi
Mkuu

12.-(1) Pale Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu itakapokuwa wazi au ikiwa Mkurugenzi Mkuu kwa sababu yoyote anashindwa kutekeleza majukumu ya ofisi yake, Waziri atamteua mtu mwingine mwenye ujuzi sahihi au uzoefu kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu kwa kipindi nafasi hiyo inapokuwa wazi au kwa kipindi hicho ambacho Mkurugenzi Mkuu ameshindwa kufanya kazi.

(2) Mtu anayekaimu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) hatakaimu kwa kipindi kinachozidi miezi sita:

Isipokuwa kwamba, Waziri anaweza kwa sababu maalumu, kuongeza kipindi kingine cha kukaimu kisichozidi miezi sita.

(3) Masharti ya kifungu kidogo (2) hayatumika ikiwa Mkurugenzi Mkuu hatakuwa ofisini kwa muda tu kutokana na majukumu ya kiofisi, katika hali hiyo, Mkurugenzi Mkuu atakasimu majukumu ya ofisi yake kwa mmoja wa watumishi walio katika ngazi ya utawala.

Wafanyakazi
wengine

13. Kwa kuzingatia sheria zinazohusu masuala ya ajira, Mkurugenzi Mkuu ataajiri wafanyakazi pale atakapona inafaa kwa ajili ya ufanisi na utekeleza kamili wa mamlaka na majukumu au kutekeleza kazi za ofisi.

Kiapo cha
kutunza siri

14.(1) Mtu yeyote ambaye si mtumishi wa Ofisi aliyejiriwa kufanya kazi yoyote inayohusu uzalishaji wa takwimu chini ya Sheria hii, atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake, kuthibitisha au kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Kamishna wa viapo kwa namna iliyowekwa katika Jedwali la Pili.

(2) Kwa madhumuni ya Kifungu kidogo cha (1), mtu atakayejiriwa kama karani wa kuhesabu watu wakati wa sensa ya watu na makazi, atathibitisha kwa maandishi kwa lugha ya Kiingereza ama ya Kiswahili na kuwasilisha uthibitisha huo kwa afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa ofisi kama ilivyo ainishwa katika Jedwali la Pili.

Maofisa
walioidhinishwa

15. Mkurugenzi Mkuu, kwa maandishi anaweza kuwateua maofisa wa ziada na kwa masharti ya muda kuwa maofisa walioidhinishwa kwa madhumuni ya kutekeleza wa majukumu ya kitakwimu chini ya Sheria hii kwa masharti na vigezo atakavyoona vinafaa.

Kutowajibishwa
kuto kufanya
kosa

16. Hakuna jambo lolote litakalofanywa na mwajiriwa wa Ofisi, ikiwa kama atalifanya au kuacha kufanya kwa nia njema katika kutekeleza majukumu au kutekeleza kazi zake kama afisa au mwajiriwa wa ofisi na mwajiriwa huyo hatawajibishwa kwa kosa lolote au hitaji la aina yoyote.

Mfumo wa
Kitaifa wa

17.(1) Kutakuwa na Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu utakaojulikana kwa kifupi NSS ambao utasimamiwa na ofisi.

Takwimu na
uratibu wake

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha 6, Ofisi itaratibu Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu kwa lengo la kuwa na mfumo wa kitakwimu unaohusiana ili kuhakikisha utumiaji unaofaa wa rasilimali zilizopo.

(3) Katika utekelezaji jukumu yake ya kuratibu chini ya kifungu hiki, Ofisi -

- (a) itatoa kanuni za maadili na kiutendaji za takwimu rasmi ambazo zitaonesha viwango vya weledi wa kufuatwa na wakala wote wa uzalishaji wa takwimu rasmi;
- (b) itaanzisha na kuendeleza kikamilifu benki ya data ya kitaifa kwa kutumia benki za data za kisékta zilizotengenezwa na wakala mbalimbali;
- (c) itaweka viwango katika ukusanyaji, uchambuzi na uchapishaji wa nakala za kitakwimu ili kuhakikisha ulinganifu katika ubora, utoshelezaji na usahihi wa taarifa za kitakwimu;
- (d) itatoa miongozo na misaada mingine inapohitajika na baadhi ya watumiaji au watoaji wa takwimu; na
- (e) itakuza ushirikiano na usawa kati ya watumiaji au watoaji wa takwimu kwa ajili ya kuepuka jitihada ziada na kuhakikisha matumizi ya rasilimali adimu.

Uhusiano na
wakala nyingine

18.-(1) Kwa kuzingatia sheria hii na bila kuathiri kifungu cha 20, Mkurugenzi Mkuu ndiye anayeweza tu kuanzisha, kubadilisha au kusitisha zoezi la ukusanyaji takwimu rasmi.

(2) Bila kujali masharti yaliyomo katika sheria nyingine yoyote hakuna mtu au wakala anayeweza kuidhinisha kuanza au kuanzisha ukusanyaji wa takwimu rasmi isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi Mkuu.

Kukasimu
madaraka ya
ukusanyaji wa
takwimu

19. Bila ya kujali masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha 18(2), Mkurugenzi Mkuu atachukuliwa kuwa amekasimu mamlaka yake kwa wakuu wa wakala ambao sheria zao zimewapa mamlaka ya kukusanya takwimu zinazohusiana na maeneo yao ya utendaji.

Takwimu rasmi

20.-(1) Takwimu Rasmi ni takwimu kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2),na zitakuwa ni takwimu zinazotengenezwa na:

- (a) Ofisi;
- (b) taasisi za Serikali; na
- (c) wakala.

(2) Takwimu zilizopo katika kifungu kidogo cha 1(c) zitakuwa na sifa za kuwa takwimu rasmi iwapo zinakidhi vigezo na viwango vilivyowekwa na Ofisi, na zimeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Kwa madhumuni ya kuhainisha, Ofisi inaweza kuweka mbinu na viwango vya kitakwimu ili kusaidia ukusanyaji na ulinganifu wa takwimu rasmi zinazozalishwa kitaifa na kimataifa.

SEHEMU YA TATU

UKUSANYAJI NA USAMBAZAJI WA TAARIFA ZA KITAKWIMU

Sensa ya watu na makazi kila miaka kumi

21.-(1) Rais anaweza, kwa Amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali kuagiza kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano kama itakavyofafanuliwa na Amri hiyo.

(2) Amri iliyotolewa chini kifungu kidogo (1), inaweza kufafanua tarehe au kipindi ambacho sensa hiyo itafanyika, taarifa zitakazokusanywa katika Sensa na kipindi ambacho sensa hiyo itafanyika.

Ukusanyaji wa takwimu nyingine

22.-(1) Ofisi inaweza kukusanya takwimu zinazohusiana na jambo lolote au mambo yote yaliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii.

(2) Ofisi inaweza kuelekeza kwamba takwimu zilizokusanywa, na taarifa nyingine yoyote rasmi ya kitakwimu, ichapishwe.

Ukusanyaji wa pamoja

23.-(1) Ofisi inaweza kuwa na makubaliano na wakala yeyote juu ya ukusanyaji wa pamoja wa takwimu zozote kwa kadiri mahitaji yatakavyojitokeza.

(2) Mfanyakazi wa wakala yeyote, kama atashiriki katika ukusanyaji au uchambuzi wa takwimu zitakazokusanywa kwa pamoja, atatoa tamko la usiri kama lilivyoelezwa chini ya kifungu cha 14, au kama litakavyoelezwa chini ya Sheria nyingine yeyote.

Utaratibu wa
Sampuli

24.-(1) Takwimu zinazohusiana na mambo yote au baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili, zinaweza kukusanywa kwa njia ya sampuli katika mahali penye rekodi zilizokamilika, pale matumizi ya utaratibu huo utaonekana kuwa unafaa.

(2) Sampuli zilizokusanywa katika kifungu kidogo cha (1) zinaweza kutumika katika majaribio ya madodoso pamoja na mchakato wa kitakwimu kabla hazijakamilika.

(3) Haitakuwa utetezi kwa mtu yeyote atakayeshindwa kujaza dodoso au kujibu maswali yeyote kwa sababu sehemu tu au kundi fulani la watu linatakiwa kujaza dodoso au kujibu maswali hayo.

Udhibiti wa
utoaji wa
taarifa

25.-(1) Taarifa zifuatazo hazitachapishwa, hazitakubalika katika ushahidi au kuonyeshwa kwa mtu yeyote ambaye si mwajiriwa katika kutekeleza majukumu yaliyomo chini ya Sheria hii, isipokuwa tu kwa kibali cha maandishi ambacho kimetolewa na mtu aliyetoa taarifa hiyo au aliyejibu swali hilo, au kama ni masuala ya kazi au shughuli, imetolewa na mtu mwenye madaraka, utawala au usimamizi wa kazi au shughuli hiyo:

- (a) taarifa binafsi au sehemu ya taarifa hiyo;
 - (b) jibu lolote lililotolewa kwa swali lolote lililoulizwa kwa madhumuni ya Sheria hii;
 - (c) taarifa, wazo au nyaraka yoyote yenye jambo lililopo kwenye madodoso au majibu ambayo yamepangwa ili kuonyesha utambulisho wa kitu hicho kwa mtu yeyote, biashara au shughuli.
- (2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika iwapo-
- (a) taarifa hizo zimetolewa na mtu, kampuni na kuchapishwa kwa marejesho, majibu, ripoti, wazo au nyaraka na kuwekwa katika kompyuta kwa ajili ya matumizi ya kawaida;
 - (b) jibu hilo au taarifa na nyaraka nyinginezo zitahitajika kwa madhumuni ya uendeshaji wa mashitaka.

Kutowajibishwa
kwa utoaji wa
taarifa

26. Bila kujali kifungu cha 23, Ofisi inaweza kutoa:
(a) taarifa zilizopatikana kutoka kwa umma chini ya Sheria yoyote au nyaraka za umma;

- (b) taarifa katika hali ya fahirisi au orodha ya majina na anuani za shughuli za watu binafsi au biashara pamoja na namba za simu ambazo wanaweza kupatikana wahusika kuhusiana na masuala ya kitakwimu, kundi la viwanda walilomo, bidhaa wanazozalisha, wanazotengeneza, wanazosafirisha, wanazotunza, wanazonunua, au wanazouza au huduma wanazozitoa wakati wa kufanya shughuli zao na idadi ya watu walioajiriwa;
- (c) maelezo ya kina ya biashara za nje, safari za meli na ndege na utunzaji wa mizigo bandarini; au
- (d) taarifa zinazohusu mamlaka za serikali za mitaa na vyombo vingine vilivyoundwa kisheria.

Utoaji wa taarifa zisizo na utambulisho

27.-(1) Kwa kuzingatia vifungu vidogo vya (2) na (3), Ofisi inaweza kutoa taarifa za kitakwimu za mtu binafsi kwa faida ya utafiti au kwa lengo la kitakwimu ikiwa kwamba:

- (a) taarifa zote za utambulisho kama vile majina na anuani ya mlalamikiwa zimeondolewa;
- (b) taarifa zimetolewa kwa namna ambayo si rahisi kuweza kujua utambulisho wa mtoaji wa taarifa au shughuli au biashara anazofanya.

(2) Mtu yeyote ambaye taarifa hizi zimetolewa kwake kwa mujibu wa kifungu hiki -

- (a) hatatakiwa kumtambulisha mtu yeyote au shughuli au biashara;
- (b) atatumia taarifa kwa utafiti au kwa madhumuni ya kitakwimu tu;
- (c) hatatoa taarifa hizo kwa mtu mwingine au taasisi;
- (d) atafuata maelekezo yoyote yatakayotolewa na Mkurugenzi Mkuu kuhusiana na taarifa hizo.

(3) Kila mtu anayejihusisha na utafiti au mradi wa kitakwimu ambao taarifa hizi zimetolewa kwa mujibu wa kifungu hiki atalazimika kutoa tamko la kutunza siri kama lilivyoanishwa katika Jedwali la Pili.

Usalama wa taarifa zilizorekodiwa

28. Ofisi itachukua hatua muhimu kuhakikisha usalama na usiri wa taarifa za Takwimu zilizokusanywa au zilizoletwa ofisini na wakala wengine katika sheria hii zinawekwa kulingana na masharti ya sheria hii.

Kuharibu fomu
na marejesho ya
taarifa binafsi

29.-(1) Ofisi au kila wakala, atatakiwa kuharibu kila sensa binafsi na fomu za tafiti na madodoso zilizotumika kwa mujibu wa Sheria hii baada ya taarifa hizo kufanyiwa kazi, kuhalalishwa na kutangazwa.

(2) Fomu binafsi za sensa na fomu za utafiti chini ya kifungu kidogo cha (1) zitaharibiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano tangu taarifa zake zilipotumika, zilipohakikiwa na kuchapishwa.

Mamlaka ya
kupata maelezo

30.-(1) Pale ambapo sensa au utafiti umefanywa au takwimu za aina yeyote zimekusanywa kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hii, afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi anaweza, kwa namna ilivyoelekezwa katika kifungu kidogo cha (2) kumtaka mtu yeyote kumpatia maelezo kama itakavyoelekezwa au kama Mkurugenzi Mkuu atakavyoona inafaa kuhusiana na sensa au ukusanyaji wa takwimu hizo.

(2) Mtu ambaye anatakiwa kutoa maelezo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), kwa kadiri ya uelewa wake, taarifa na kuamini, atatakiwa kujaza fomu hizo, kutoa marejesho hayo, kujibu maswali hayo na kutoa taarifa hizo kwa namna na ndani ya muda kama utakavyokuwa umeelekezwa na afisa aliyeruhusiwa au mtumishi wa Ofisi.

(3) Afisa aliyeidhinishwa au Mtumishi wa Ofisi anaweza, katika muda wowote unaofaa na baada ya kujitambulisha:

(a) kuhusiana na zoezi la sensa au tafiti, kuingia na kufanya ukaguzi katika jengo lolote ikiwa ni eneo lolote ikijumuisha nyumba; na

(b) kuhusiana na ukusanyaji wa takwimu nyingine ataingia na kukagua katika jengo lolote pale ambapo shughuli zinazotoa faida au riba zinafanywa, na kwa njia nyingine anaweza kuhoji kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya kuchukua sensa au ukusanya takwimu kama itakavyokuwa.

Upatikanaji wa
kumbukumbu

31.-(1) Pale ambapo Mkurugenzi Mkuu anaona kwamba ukusanyaji wa takwimu zinazohusiana na jambo lolote zinaweza kupatikana kutoka kwenye taasisi yoyote ya Serikali, wakala au mtumiaji au mzalishaji wa takwimu, atatoa idhini kwa afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi kwa madhumuni ya kupata taarifa inayohitajika.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), taarifa zilizopatikana zitahusu masuala ya ukusanyaji wa takwimu zilizothibitishwa au kuelekezwa au kwa ajili ya kumaliza au kukusanya takwimu.

**SEHEMU YA NNE
MASUALA YA FEDHA**

Vyanzo vya
mapato

- 32.** Vyanzo vya fedha na raslimali za Ofisi zitatokana na-
- (a) fedha inayotengwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi;
 - (b) fedha inayopatikana kutokana na mauzo ya bidhaa na huduma zinazotolewa na Ofisi;
 - (c) kiasi cha fedha kilichokopwa, kilichopokelewa au kupatikana kwenye Ofisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake; na
 - (d) michango, misaada na zawadi inayopokelewa na Ofisi kutoka kwa mtu au taasisi yeyote.

Makadirio

- 33.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, si zaidi miezi mitatu kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, atatayarisha na kuwasilisha kwenye Bodi mpango kazi na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha unaokuja.
- (2) Bodi itawasilisha kwa Waziri, mpango kazi na makadirio kwa ajili ya idhini yake.
- (3) Hakuna matumizi yatakayofanywa kwa kutumia fedha za Ofisi isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya madirio ya matumizi yaliyoidhinishwa na Waziri chini ya kifungu kidogo cha (2).

Hesabu

- 34.**-(1) Ofisi itatunza vitabu vya hesabu-
- (2) Kufuatana na maelekezo yoyote yaliyotolewa na Bodi, Mkurugenzi Mkuu atatayarisha maelezo ya kila mwaka wa fedha, kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha, yatakayojumuisha taarifa ya utendaji wa Ofisi ya mwaka huo wa fedha.
- (3) Taarifa zilizoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha pili zitakuwa na-
- (a) mizania na taarifa ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa ajili ya mwaka huo wa fedha; na
 - (b) taarifa nyingine yoyote ya maandishi inayohusu masuala ya fedha za Ofisi kama ambavyo Waziri anaweza kuhitaji.

Ukaguzi

35.-(1) Mahesabu ya Ofisi ya kila mwaka wa fedha yatakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu au Mkaguzi atakayeteuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu.

(2) Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi mitatu baada ya kufunga mahesabu ya mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu kwa ajili ya ukaguzi wa taarifa ya hesabu kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 34 cha Sheria hii.

(3) Mkurugenzi Mkuu mapema iwezekanavyo kwa kipindi kisichozidi miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi kutoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu, atawasilisha maelezo ya taarifa ya fedha kwa Waziri iliyokaguliwa pamoja na taarifa ya Mkaguzi.

Taarifa ya mwaka ya utekelezaji

36. Bodi itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ndani ya miezi mitatu baada ya kufunga hesabu za fedha za kila mwaka, taarifa ya mwaka juu ya utendaji wa Ofisi ndani ya mwaka huo wa fedha.

SEHEMU YA TANO MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

37.-(1) Mtu yeyote ambaye-

- (a) kwa nafasi ya kazi yake anapata taarifa yoyote inayoweza kuathiri thamani yoyote ya soko la hisa au amana zingine, riba, bidhaa au kitu na kabla ya taarifa hizo hazijatolewa kwa umma, atatumia moja kwa moja taarifa hizo au kwa kificho kwa manufaa yake binafsi;
- (b) bila ya mamlaka halali, anachapisha au kutoa kwa mtu mwingine yeyote taarifa alizozipata kwa mujibu wa kazi yake kinyume na utaratibu wa kawaida wa ajira;
- (c) anatelekeza jukumu lake au kwa makusudi anatoa tamko lolote, kauli au rejesho katika utekelezaji wa kazi yake, au anakusanya na kuzitoa taarifa zozote za uongo za takwimu;
- (d) kwa kujifanya anatimiza majukumu yake anapata au anaomba kupatiwa taarifa ambayo hajaidhinishwa kuipata;
- (e) kutokana au kuhusiana na kazi yake chini ya Sheria hii, bila idhini anaomba, anapokea au kuchukua malipo au zawadi kutoka kwa mtu yeyote isipokuwa mtumishi wa Umma aliyeidhinishwa,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa faini isiyopungua milioni mbili au kifungo cha muda usiopungua miezi sita, au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote ambaye anamiliki taarifa yoyote ya kitakwimu, ambayo kwa ufahamu wake anajua zimetolewa kinyume na masharti ya sheria hii, anachapisha au anasambaza kwa watu wengine taarifa hizo, anatenda kosa, na akipatikana na hatia atahukumiwa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo cha muda usiopungua miezi kumi na mbili, au vyote kwa pamoja.

(3) Mtu yeyote ambaye-

(a) anamchelewesha au anamzuia afisa yeyote aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi katika kufanya kazi yoyote au kutimiza mamlaka yake yaliyowekwa chini ya Sheria hii;

(b) anayekataa au kwa makusudi anaacha:

(i) kukamilisha na kusambaza ndani ya muda uliopangwa taarifa zinazotakiwa katika marejesho, fomu au nyaraka yoyote iliyoachiwa au kutumwa kwake; au

(ii) kujibu swali lolote au hoja iliyoelekezwa kwake chini Sheria hii;

(c) kwa kujua anatoa kauli isiyo ya kweli katika marejesho, fomu au nyaraka yeyote aliyoijsa kwa mujibu wa Sheria hii, au katika kujibu swali lolote au hoja yoyote iliyoelekezwa kwake chini ya Sheria hii;

(d) bila mamlaka ya kisheria, anaharibu, kuchafua au kuchana marejesho, fomu au nyaraka yoyote yenye taarifa zilizokusanywa kwa mujibu wa Sheria hii;

(e) akijua si afisa aliyeidhinishwa au mfanyakazi wa Ofisi, anajipa sifa au kujitambulisha kuwa ni mfanyakazi wa Ofisi;

(f) anamhamasisha au anamshauri mtu mwingine yeyote asishiriki kwenye shughuli inayohusiana na ukusanyaji wa taarifa chini ya Sheria hii;

(g) anafanya kitu chochote ambacho hana haki ya kukifanya;

(h) anakataa bila sababu ya msingi kutoa kumbukumbu au nyaraka kwa mujibu wa vifungu vya 30 na 31;

(i) anakiuka masharti ya kifungu chochote cha sheria hii ambacho hakuna adhabu mahsusi iliyotajwa,

anatenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo cha muda usiopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(4) Chombo chochote cha habari ambacho kinachapisha taarifa za kitakwimu za uongo au za upotoshaji, au kinatangaza kipindi chochote kinachohusu shughuli za ukusanywaji wa taarifa ambayo imefanywa au inafanywa na Ofisi, na hatimaye kusababisha wananchi wasishiriki kwenye shughuli hiyo ya ukusanywaji wa taarifa au wasishirikiane na maafisa wa Ofisi, kinatenda kosa na kitakapotywa hatiani kitawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kifungo cha muda usiopungua miezi kumi na mbili au vyote viwili.

(5) Mtu yeyote au wakala ambaye, bila idhini ya kisheria kutoka kwa Ofisi, anachapisha au anasambaza taarifa za kitakwimu ambazo zinaweza kusababisha upotoshwaji wa taarifa husika, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kifungo cha muda usiopungua miaka miezi ishirini na nne.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “chombo cha habari” kinajumuisha kituo cha radio, kituo cha televisheni, gazeti au jarida, tovuti au chombo kingine chochote cha habari.

SEHEMU YA SITA MASUALA YA JUMLA

Kanuni

38. Waziri anaweza, kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, kutengeneza Kanuni za-

- (a) kuelezea namna ambayo mfumo wa kitaifa wa takwimu itakavyoratibiwa;
- (b) kutaja kiwango cha ada na tozo itakayolipwa kwa ajili ya taarifa maalum au ripoti iliyotolewa au huduma maalumu za takwimu zilizotolewa ;
- (c) kuongeza au kufuta au kubadili jambo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili; na
- (d) masuala yote ambayo ni muhimu kulingana na sheria ya kudhibiti masuala ya takwimu nchini kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

Kufuta na
kuhifadhi

39.-(1) Sheria ya Takwimu imefutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)-

- (a) jambo lolote lililofanywa au hatua yoyote iliyochukuliwa au kukusudiwa kuchukuliwa chini ya Sheria iliyofutwa, itachukuliwa kuwa imefanywa chini ya Sheria hii;
- (b) uteuzi wowote uliofanywa chini ya Sheria iliyofutwa na ambao haujatenguliwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii utachukuliwa kuwa umefanywa chini ya Sheria hii na utabakia kuwa na nguvu kisheria hadi pale utakapotenguliwa au uteuzi mpya utakapofanyika chini ya Sheria hii; na
- (c) mwenendo wowote wa kisheria uliofanywa na amri zilizotolewa chini ya Sheria iliyofutwa utaendelea na kuchukuliwa kwamba ni mwenendo au amri zilizofanywa chini ya sheria hii.

Kukinzana na
Sheria nyingine

40. Pale masharti ya Sheria hii yatakinzana au kutofautiana na masharti ya Sheria nyingine inayohusu masuala ya takwimu, masharti ya Sheria hii yatakuwa na nguvu kulingana na tofauti hiyo.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kifungu 7)

Muda wa
uteuzi

1.-(1) Kila mjumbe wa Bodi atakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1) ya aya hii, mjumbe anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa taarifa kimaandishi kwa mamlaka ya uteuzi na tangu tarehe hiyo iliyoainishwa kwenye taarifa, mjumbe huyo atakoma kuwa mjumbe, au, iwapo hakuna tarehe iliyoainishwa kwenye taarifa hiyo, mjumbe huyo atakoma kuwa mjumbe kuanzia tarehe ambayo mamlaka ya uteuzi imepokea taarifa hiyo.

(3) Mtu ambaye ni mjumbe kutokana na kushika madaraka katika ofisi yoyote atakoma kuwa mjumbe baada ya kuacha kushika madaraka katika ofisi ambayo kwa wadhifa huo amekuwa mjumbe.

Kufuta uteuzi

2. Pale ambapo mjumbe wa Bodi anashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya Bodi mfululizo bila sababu za msingi, Bodi itaishauri mamlaka ya uteuzi kuhusu suala hili na mamlaka ya uteuzi inaweza kufuta uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwingine badala yake.

Ukomo wa
kuwa
mjumbe

3. Iwapo mjumbe yeyote wa Bodi anakoma kuwa mjumbe kwa sababu ya kujiuzulu au kifo au kwa ya kushindwa kutekeleza majukumu yake kama mjumbe kwa sababu ya kutokuwepo ndani ya Jamhuri ya Muungano au kwa sababu ya udhaifu wa mwili au akili au iwapo mamlaka ya uteuzi inafuta uteuzi wake chini ya aya ya 2, mamlaka ya uteuzi inaweza kuteua mjumbe mwingine badala yake na mjumbe atakaye teuliwa kwa mujibu wa Jedwali hili atakuwepo madarakani kwa muda uliobakia wa mjumbe aliyemtangulia.

Makamu
Mwenyekiti

4. Bodi itamchagua mmoja kati ya wajumbe wake kuwa Makamu-Mwenyekiti na mjumbe yeyote atakayechaguliwa kuwa Makamu-Mwenyekiti, na kwa kuendelea kwake kuwa mjumbe atashika madaraka ya Makamu-Mwenyekiti kwa muda utakaopangwa na Bodi na atastahili kuchaguliwa tena baada ya muda huo kuisha.

Mamlaka ya
Mwenyekiti
na Makamu
Mwenyekiti

5.-(1) Mwenyekiti ataongoza mikutano yote ya Bodi.

(2) Iwapo katika mkutano wowote wa Bodi Mwenyekiti hata kuwepo, Makamu-Mwenyekiti ataongoza kikao hicho.

(3) Iwapo Mwenyekiti na Makamu-Mwenyekiti hawapo katika kikao chochote cha Bodi, wajumbe waliopo, wataamchagua Mwenyekiti wa muda kutoka miongoni mwao kuongoza kikao.

(4) Mwenyekiti, Makamu-Mwenyekiti au Mwenyekiti wa muda anayeongoza kikao chochote cha Bodi, atakuwa na haki ya kupiga kura, na inapotokea uwiano wa kura atakuwa na kura ya turufu mbali na kura yake ya kawaida.

Mikutano na
taratibu za
Bodi

6.-(1) Kikao cha kawaida cha Bodi kitaitishwa na Mwenyekiti na taarifa inayotaja sehemu, tarehe na muda wa kikao itatumwa kwa kila mjumbe mahala pake pa kawaida pa kazi au makazi kwa siku zisizopungua siku 14 kabla yatarehe ya kikao hicho.

(2) Bodi itafanya vikao vya kawaida vinne kwa mwaka, lakini Mwenyekiti anaweza akaitisha kikao cha dharura endapo hitaji la kufanya hivyo litajitokeza.

(3) Mwenyekiti wa Bodi anaweza kumwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika mjadala wa Bodi na mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi

7.-(1) Mwenyekiti na wajumbe wengine watatu wataunda akidi ya mkutano wa Bodi.

(2) Iwapo Mwenyekiti kuwepo kwenye kikao cha Bodi, wajumbe waliopo wataamchagua mmoja wao kuwa Mwenyekiti wa muda wa kikao hicho.

Uamuzi kwa
njia ya
maandishi

8.-(1) Bila kujali aya cha 7, kwa maelekezo ya Mwenyekiti uamuzi unaweza kufanywa na Bodi bila kikao kwa kwa kugawa nakala husika kwa wajumbe wote ili kutoa maoni yao kwa maandishi.

(2) Mjumbe yeyote atakuwa na haki ya kutaka uamuzi wowote unaokusudiwa kufanywa usifanyike na suala hilo lijadiliwe katika kikao cha Bodi.

Muhtasari wa
mkutano

9. Muhtasari wa kila kikao cha Bodi utatunzwa na utathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti wa kikao hicho.

Uhalali wa matumizi ya lakiri

10. Lakiri ya Bodi haitawekwa kwenye hati, nyaraka na miongozo mingine isipokuwa mbele ya Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu, au Mwenyekiti au Mkurugenzi Mkuu na mjumbe mwingine mmoja ambaye atateuliwa na Bodi.

Uthibitishaji wa nyaraka

11. Nyaraka zozote ambazo zinaihusu Bodi mbali na nyaraka nyingine zinazohitajika kisheria kuwekwa lakiri na maamuzi yote ya Bodi, inaweza kuthibitishwa kwa kusainiwa na Mkurugenzi Mkuu au ofisa mwingine aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa niaba yake.

Uhalali wa vikao

12. Hakuna jambo au mwenendo wa Bodi kitachokuwa batili kwa sababu ya idadi ya wajumbe kutokamilika wakati wa kikao hicho kwa sababu ya idadi pungufu ya wajumbe wakati wa kufanya jambo hilo au mwenendo huo au kasoro zozote katika uteuzi wa mjumbe yeyote au kwamba mjumbe yeyote kwa wakati huo hakuwa na sifa au hastahili kuwa mjumbe.

Bodi kusimamia shughuli zake

13. Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili Bodi inaweza kusimamia shughuli zake.

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 14)

Aidha;

Mimi.....naapa/nathibitisha kwamba nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu na uadilifu kama.....kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Takwimu, na kwamba sitatoa taarifa yoyote ninayoipata kutokana na kazi yangu hii bila kibali halali.

.....
SAHIHI

Kiapo kimetolewa/uthibisho umetolewa mbele yangu leo tarehe.....Mwezi.....Mwaka.....

.....
KAMISHNA WA VIAPO

Au;

Mimi.....natamka kwamba nitakuwa mwaminifu na muadilifu katika kutekeleza majukumu yangu kama Mdadisi katika Sensa ya Watu kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Takwimu, 2010, na kwamba sitatoa taarifa yoyote ninayoipata kutokana na kazi yangu hii bila kibali halali.

.....
SAHIHI

Kiapo kimetolewa mbele yangu tareheMwezi.....Mwaka.....

Jina

Wadhifa.....

Anuani.....

Sahihi.....

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya vifungu vya 22 na 23)

1. Sensa ya Watu na Makazi
2. Usajili wa Vifo, Vizazi na Matukio ya Jamii
3. Uhamiaji
4. Biashara ya Nje, Urari wa Biashara na Utalii
5. Taarifa za Kiuchumi
6. Kilimo
7. Ujenzi
8. Viwanda (Madini, Bidhaa za Viwandani, Umeme na Maji)
9. Soko la Ajira
10. Fedha za Serikali, Sera za Kifedha na Sekta ya Umma
11. Umaskini na mgawanyo wa mapato
12. Masuala ya Jamii, Elimu, shughuli za Kazi na Viwanda pamoja na Vyama vya Waajiri, Waajiri wa na Watu Wengine kwa Ujumla
13. Benki, Bima na Masuala ya Fedha kwa Ujumla
14. Biashara na Shughuli za Kitaalam
15. Biashara ya Ndani ya jumla na Rejareja
16. Elimu na Afya
17. Usafiri na Mawasiliano katika sekta zote za Usafiri wa Nchi Kavu, Maji na angani
18. Madhara, ajali, na fidia
19. Akiba ya bidhaa za viwandani
20. Bahati Nasibu, misaada ya kujitolea na makusanyo mengine na umma
21. Umiliki wa ardhi, makazi na matumizi ya ardhi
22. Mamlaka ya Serikali za Mitaa
23. Uharifu na haki
24. Mazingira
25. Utafiti katika ngazi ya Kaya Binafsi
26. Biashara ndogo ndogo
27. Habari, Teknojia na Mawasiliano
28. Jamii, Ustawi wa Jamii, na huduma Binafsi
29. Jinsia
30. Halim ya Hewa
31. Biashara

32. Bei
33. Nishati
34. Uwekezaji
35. Maji Safi naMaji Taka
36. Utafiti na Kuendeleza Ugunduzi
37. Vito vya Thamani
38. Utawala
39. Matangazo
40. Sehemu zinazotoa huduma za uzalishaji

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Takwimu, Sura 351 na kutungwa Sheria mpya ya Takwimu. Madhumuni na mapendekezo haya ni kujibu udhaifu na uzoefu uliokuwepo katika utekelezaji wa kukusanyaji wa takwimu hususan katika matumizi sahihi ya takwimu nchini. Kwa hiyo Sheria mpya inayopendekezwa itatoa madaraka kamili kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuwa kitovu cha utoaji wa takwimu nchini.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu Sita. Sehemu ya Kwanza inatoa masharti ya utangulizi wa Muswada pamoja na jina la Muswada husika na ufafanuzi wa baadhi ya maneno au misamiati iliyotumika katika Muswada huu.

Sehemu ya Pili, inapendekeza kuendelea kuwepo Ofisi ya Taifa ya Takwimu kama chombo huru pamoja na kubainisha majukumu ya Ofisi hii ikiwa ni pamoja na mamlaka ya kuratibu shughuli zote za utoaji wa takwimu rasmi nchini. Sehemu hii pia inaanzisha wa Bodi ya Usimamizi wa Takwimu, uteuzi na majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na masuala yanayohusu utendaji wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa jumla.

Sehemu ya Tatu, inaweka masharti kuhusu suala la ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za kitakwimu. Sehemu hii pia inaelezea kuhusu masuala ya Sensa ya Watu na Makazi pamoja na masuala yanayohusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kitakwimu yanafafanuliwa katika sehemu hii.

Sehemu ya Nne, inapendekeza masharti mbalimbali yanayohusiana na fedha za Ofisi ya Taifa za Takwimu, vyanzo vya fedha vya Mfuko, makadirio na uwasilishwaji wa Ripoti ya mwaka ya utendaji kwa Waziri.

Sehemu ya Tano, inaelezea makosa yote yanayohusu masuala ya takwimu ikiwa ni pamoja na makosa yanayohusu utoaji wa takwimu zisizo rasmi na zinazoweza kuleta

migogoro katika jamii. Aidha, sehemu hii inaainisha adhabu mbalimbali zitakazotolewa kulingana na makosa hayo.

Sehemu ya Sita na ya mwisho inahusu masuala ya jumla ikiwa ni pamoja na kufutwa kwa Sheria ya Takwimu Sura 351 mambo yanayohitaji kuhuishwa chini ya Sheria inayofutwa na mamlaka ya kuandaa Kanuni chini ya Sheria hii.

Dar es Salaam,
4 Juni, 2013

WILLIAM A. MGIMWA
Waziri wa Fedha